© Manhaj ya Salafi 2002. www.manhajyasalafi.com

Sehemu ya Kwanza: [Vidokezo Kutoka Katika "Fadhaa-il Durood"]

Sifa zote njema ni zenye kumthubutukia Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah). Tunamsifu Yeye, Tunamtaka msaada na Kumuomba msamaha. Tunajilinda Kwake Yeye, Alie Juu zaidi kutokana na maovu ya nafsi zetu na vitendo vyetu viovu. Yeyote ambae alie-ongozwa na Mwenyezi Mungu, hapana yoyote awezae kumpotoa na Yeyote ambae alie-potolewa na Mwenyezi Mungu, hapana yoyote awezae kumuongoza. Nashuhudia yakwamba hapana mola wa kweli apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Peke yake, asie na msaidizi wala mshirika. Na pia, nashuhudia yakwamba Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam) ni Mtumwa na Mjumbe wake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) Azifikilize Amani na Baraka Zake juu ya mjumbe wake wa mwisho Muhammad, na juu ya ahli zake, maswahaba zake watukufu na wafuasi wao wote.

Mwanzo kabisa:

Maneno yalio ya kweli ni Qur'aan, Neno la Mwenyezi Mungu na uongofu ulio bora ni wa Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam) . Na yalio movu mno katika dini hii yetu ni mambo ya uzushi na kila uzushi ni Bid'ah na kila Bid'ah ni upotofu na kila upotofu mwisho wake ni motoni.

Kurasa hii ambayo ni ya kwanza katika mfululizo unaokusanywa ili kumtanabahisha Muislamu mwenye hamu ya kutaka kuujua Uislamu. Uislamu kama ulivyoteremshwa na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) kwa Mjumbe wake wa mwisho (Sallallahu 'alayhi wasallam); ulioepukana na mageuzi yoyote, upungufu wowote na nyongeza za aina yoyote. Lakini leo kuna kivuli chenye giza kilichotandazwa juu ya haki. Shirk na Bid'ah zimewang'ata Waislamu baraabara. Baatil imejivika vazi la haki na wajinga wakayavaa majoho ya wanavyuoni.

Uzalendo wa kwenye makundi, mapote na vyama umezigawanya nyoyo za Waislamu. Sheria na kanuni za mapote na vyama vyao wamezifanya kuwa ni bora kuliko Sheria za Qur'aan na Sunnah zilizo Saheeh. Tafseer za Aya za Qur'aan zilizo baatil na mikasa ya Seerah zinazoafikiana na maazimio ya vyama zimekithiri siku hizi.

Moja katika makundi hayo ni "Jamaa'at at-Tableegh" au "Tableeghi Jamaat." hili ni pote lililoanzishwa kwenye miaka ya 1920s. Waislamu wengi wanadai yakwamba wakoloni kutoka Uingereza ndio walioibuni Jamaa'ah hii kwa min-ajil ya kuzigawanya nyoyo za Waislamu kwa 'Aqeedah mbovu na kuvunja hima ya Jihaad lakini wafuasi halisi wa Qur'aan, Sunnah na Manhaj ya watangulizi wetu wema hawpendelei kuwa na dhana za fitina na badala yake hutizama yale yalio wazi na uhakika. Tableeghi Jamaat wanatoa mafunzo yao kutoka kwenye Kitabu kiitwacho "Fadhaa-il A'maal" (wema wa amali) kilichoandikwa na Muhammad Zakaria Kandalvi baada ya kuraiwa na kuhimizwa na Ashraf 'Ali Thanvi, hao wawili kama wajulikanavyo kuwa ni vigogo vya pote la Deobandh kutoka India.

Leo, hawa Tableeghi Jamaat wanaofikiriwa kuwa ni "pote la mahubiri" kubwa zaidi linalo-walingania Waislamu Kuswali, kufunga, Hajj n.k. Wale wenye kujinasibisha na pote hili **WANADAI** eti kitabu hicho "Fadhaa-il A'maal" (pia kinaitwa Tableeghi Nisaab) ni mkusanyiko wa Aya mbalimbali kutoka katika Qur'aan na Ahaadeeth zinazoeleza kuhusu wema na malipo makubwa kuhusiana na Hajj, Zakaah, Salaah, Dhikr n.k. **LAKINI** uchunguzi uliofanywa kuhusu kitabu hiki kulingana na muangaza wa Qur'aan na Sunnah zilizo Saheeh umedhihirisha mafunzo ya kutisha ya **SHIRK**,uzushi,urongo wa kumzulia Mtume Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam), utwevu juu ya watu wema wa qarne ya maswahaba watukufu na wanavyuoni. Amma kweli, kwa jina la mapenzi ya Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) na watu wema, Sheitaan

amewashawishi hawa wenye firqah hii na akawavutia kwenye SHIRK na KUFR- mambo ambayo wamejipofusha nayo.

Kurasa hii na utafiti zaidi kwenye kitabu hicho utaonyesha hoja zisizo-kanushika pamoja na kumbukumbu zenye kusihi ili kuthibitisha, Insha-Allah, yakwamba yale mafunzo kwenye kitabu hicho si chochote bali ni 'Ibaadah za makaburi, maombi kwa asiekuwa Mwenyezi Mungu, na kuthibitisha yakwamba mafunzo ya 'aqeedah (Imaan) kwenye kitabu hicho haina uhusiano wowote na Uislamu lakini ni Imani za asiemuamini Mwenyezi Mungu (upagani). Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) Atulinde na hayo.

Angalia: Chapa ya Fadhaa-il A'maal (Chapa ya Urdu) ambayo itakayotumiwa imechapishwa kutoka:

Idara Irshaad-e-Diniaat Pvt. Ltd.
Nizamuddin, No-13
Delhi, India

Iwapo huna chapa hiyo iliyotajwa hapo juu, hiyo uliyonayo nyumbani itahitilafiana kwa kurasa chache nyuma au mbele.

Vilevile Hikaayat zilizotajwa baada ya Fadhaa-il Durood katika Fadhaa-il A'maal zina idadi sawasawa kwenye chapa zote. Neno hilo "Hikayat" limefasiriwa kama "tukio" kwenye kurasa hii.

Shirk kwenye "Fadhaa-il Durood" (Amali za kumswalia Mtume) - [Mlango wa mwisho katika Fadhaa-il A'maal]

[Amma kuhusu Kutuma Swala na Salamu kwa Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam), kwa hakika hilo ni miongoni mwa 'amali njema na kitendo kinachostahili sifa. Na jinsi ya Kutuma Swala na Salamu tumefundishwa kutoka katika Sunnah zilizo saheeh, na ni jambo lililo-epushwa na urongo na uzushi ambao mutakao usoma kwenye kurasa hii, kutoka katika vitabu vya Jamaa'at-ut-Tableegh. Jambo muhimu utaona hapa ni uzushi mkubwa na kuongeza yasokuwemo, kuhusiana na suala la Kutuma Swala na Salamu kwa Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) kama yatakavyo-dhihiri kwa njia zisofichika.

1) 'Aqeedah ya 'Ibaadah za makaburi katika "Fadhaa-il Durood"

Ni Imani ya kila Muislamu yakwamba kumuomba asiekuwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) (k.m malaika, walii, mitume walokufa, wanavyuoni) katika wakati wa dhiki au raha kwa kutarajia yakwamba kiumbe huyo anao uwezo wa kukuondolea dhiki na maafa, au yakwamba kwa kuhusika kwa kiumbe huyo, dhiki na maafa huondoka, ni kitendo cha Shirk. Akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) katika Qur'aan Tukufu (kama ilivyo fasiriwa):

وَلَا تَدۡعُ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَۖ فَإِن فَعَلۡتَ فَإِنَّكَ إِذٗا مِّنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ١٠٦

"Na (nikaambiwa) 'Wala usiwaabudu badala ya Mwenyezi Mungu wale ambao hawakufai (unapowaabudu) wala hawakudhuru (unapowaacha kuwaabudu). Basi ukifanya, utakuwa miongoni mwa madhalimu (wa nafsi zao).'" [Soorah Yoonus, Aayah 106]

Na pia kutoka katika Ahaadeeth Saheeh. Akapokea 'Aaisha (Radhiallahu 'anha) kutoka katika Hadeeth iliyopokewa na Bukhari na Muslim: "Umm Salamah alimwambia Mtume (Sal-Allaahu

`alayhi wa sallam) yakwamba alipokuwa Abyssinia (Habashah) aliliona kanisa lililojaa picha na masanamu. Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) akamwambia: **"Anapokufa mtu mwema au walii miongoni mwao, wao hujenga mahali pa kufanya 'Ibaadah juu ya kaburi lake na hueka kila aina ya picha na masanamu. Wao ni viumbe waovu mno mbele ya Mwenyezi Mungu. Huchanganya maovu ya aina mbili; kufanya 'Ibaadah katika makaburi na kuchonga picha zilizonakishiwa na masanamu."**

Vilevile ikapokewa na Imaam al-Bukhari na Muslim kutoka kwa 'Aaisha (Radhiallahu 'anha) kuwa amesema: "Mauti yalipomfikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) alianza kujipangusa uso wake kwa kitambara (tandiko la kitanda), (alikuwa akijifunika na mara akijifunua kwa ajili ya machungu), basi akasema (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam), akiwa katika hali hii: **"Laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya Mayahudi na Manasara kwa kuyafanya makaburi ya Mitume yao kuwa mahali pa 'Ibaadah"**

Kwahivyo, Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) akawaonya watu kuhusu vitendo vyao.

Imaam Muslim akapokea kutoka kwa Jundub bin 'Abdullah (Radhiallahu 'anhu) aliesema: Nilimsikia Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) akisema siku tano kabla ya mauti yake: **"Mimi nina khiyari na ruhusa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ya kumfanya yeyote miongoni mwenu kuwa ni Khaleel (urafiki wa chanda na pete) wangu. Kwa hakika, Mwenyezi Mungu amenifanya mimi kuwa ni Khaleel Wake kama vile Alivyomfanya Ibraaheem (`alayhis-salaam) kuwa Khaleel. Lau ningelimfanya yeyote miongoni mwa Ummah wangu kuwa ni Khaleel, basi ningelimfanya Abu Bakar (radhi-yallaahu 'anhu) kuwa ni Khaleel. Jitahadharini! Wale walokuja kabla yenu, walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume yao kuwa ni sehemu za 'Ibaadah. Tahadharini! Musiyafanye makaburi (yoyote) kuwa ni sehemu za 'Ibaadah. Mimi nawakataza kufanya hivyo."**

Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) alilikataza jambo hili mwishoni mwa maisha yake. Baada ya hapo (kuharamisha kuyafanya makaburi kuwa sehemu za 'Ibaadah), alimlaani yeyote mwenye kufanya kitendo kama hicho kuhusiana na suala hili. Akasema Imaam Abu Haneefah:

Haijuzu kwa mtu yoyote kumuomba Mwenyezi Mungu, isipokuwa kwa Majina yake, na iwe ni kwa maombi Aliyoyaruhusu na Kutuamrisha Yeye Mwenyewe kama ilivyo katika maneno Yake (kama ilivyofasiriwa):

وَلِلَّهِ ٱلْأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ فَٱدْعُوهُ بِهَا ۖ وَذَرُوا۟ ٱلَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِىٓ أَسْمَٰٓئِهِۦ ۚ
سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٨٠﴾

"Na Mwenyezi Mungu ana Majina mazuri mazuri; muombeni kwayo. Na waacheni wale wanaoharibu Utakatifu wa Majina Yake. Karibuni hivi watalipwa yale waliyokuwa wakiyatenda." [Soorah al-A'raaf, Aayah 180], [ad-Durrul-Mukhtaar ma'a Haashiyah Raddul-Mukhtaar (6/396-397)]

Akasema Abu Haneefah: Ni jambo la kuchukiza kwa mwenye kuomba kusema: "Nakuomba Mwenyezi Mungu kwa haki ya fulani na fulani" au, "Kwa haki ya Mitume Wako na wajumbe wako, na kwa haki ya Nyumba Tukufu na mahali patakatifu" [Sharhul-'Aqeedatut-Tahaawiyyah (uk. 234) na Ithaafus-Saadaatul-Mustaqeem (2/285) na Sharhul-Fiqhil-Akbar (uk. 198) kitabu cha al-Qaaree]

Akasema tena Imaam Abu Haneefah:

Haijuzu kwa mtu yoyote kumuomba Mwenyezi Mungu, isipokuwa kwa Majina yake na inachukiza zaidi atakaposema, "Kwa Utukufu wa Jaha ya Kiti Chako" au, "Kwa haki ya Viumbe Vyako". [al-Fiqhul-Absat (uk. 56)]

Hayo ndiyo tuyajuayo kuhusiana na 'Ibaadah au maombi ya kwenye makaburi na kupeleka maombi kwa asiekuwa Mwenyezi Mungu. Tumeyapata mafunzo hayo kutoka kwenye Qur'aan na Sunnah zilizo saheeh. Lakini, hebu tusomeni aloyaandika Muhammad Zakaria Kandalvi katika Fadhaa-il A'maal. Katika Fadhaa-il Durood, uk.97, Tukio la (Hikayat) 35: (Wanadai yakwamba) Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) amesema: "Mwenye haja na kitu chochote kutoka kwa mtu yoyote basi naende katika kaburi lake kisha akiombe kitu hicho kwa Mwenyezi Mungu"

Pia katika Ukurasa 109, Tukio la (Hikayat) - 48, Fadhaa-il Durood (Mlango wa mwisho katika Fadhaa-il A'maal, Vol.I): "Sh. Abu Khair Qattah amesema: Nilikwenda Madeenah na nikakaa hapo kwa muda wa siku tano lakini sikutosheka na kufurahika kama nilivyotarajia. Nikenda kwenye makaburi ya Mtume, Hadhrat Abu Bakar na Hadhrat 'Umar kisha nikasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, usiku wa leo mimi ni mgeni wako". Kisha nikaondoka hapo nikaenda kulala nyuma ya minbar. Nikaota nikiwa usingizini yakwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu akiwa na Abu Bakar upande wake wa kulia, 'Umar upande wake wa kushoto na 'Alee akiwa mbele yao wote. Kisha Hadhrat 'Alee akanitikisa na kuniambia yakwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu amekuja kunitembelea mimi. Palepale nikaamka na kumbusu Mtume katikati ya macho yake. Mtume wa Mwenyezi Mungu akanipa kipande cha mkate ambacho nilikila nusu yake na nilipoamka ile sehemu nyengine ya nusu ilikuwa mkononi mwangu".

Ni kitu gani ambacho Zakaria Kandalvi anachotaka kututhibitishia kwa kupitia hivi visa viovu vya uzushi. Eti kufanya maombi karibu na makaburi hujibiwa kwa kutembelewa na Mtume mwenyewe na kutuzwa kipande cha mkate. Na jee, mambo yatokeayo ndani ya ndoto hubakia baada ya ndoto kumalizika? Laa! Lakini Zakaria Kandalvi anataka kuwapa wasomi wake fikra yakwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu na wale Maswahaba watukufu walimtembelea Sh.Qattah kikweli na sio ndoto tu. Hivi visa viwili vinatosha kuthibitisha mafunzo ya 'Ibaadah za makaburi katika Fadhaa-il A'maal. Mwanzo kabisa, "Shaykh al-Hadeeth" Muhammad Zakaria Kandalvi ameizua hadeeth hiyo halafu pamoja na kisa chote hicho. Lakini huu sio mwisho wa Shirk na urongo ulioko katika Fadhaail A'maal. Ndio mwanzo twaanza.

Kwa hakika Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) amekuja kutuonya vikali kuhusu Shirk, na isitoshe, akaifunga milango yote yenye kutuelekeza kwenye njia za Shirk - kwahivyo akatukataza kuelekea makaburi tunaposwali, akatukataza kupindukia mipaka katika kuwasifu watu kupita kiasi, akatukataza kuvaa talasimu (hirizi), akatukataza kula viapo kwa asiekuwa Mwenyezi Mungu, akatukataza kujenga misikiti juu ya makaburi na kuyajengea makaburi, akaamrisha kuzitokomeza picha, kuvunja masanamu na kuyasawazisha makaburi (yaliyo nyanyuliwa) kwenye ardhi. Kisha wakaja watu mfano wa Muhammad Zakaria Kandalvi, akazua mambo ya kushangaza, akatamka maneno ya urongo kupita kiasi dhidi ya dini hii na dhidi ya Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) bila ya ushahidi wowote wala isnaad (silsila ya upokezi) ya kumbukumbu na AKAZIFUNGULIA MLANGO njia zilezile za kutuelekeza kwenye Shirk zilizofungwa na Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam)! Na kwa hakika, katika kuhadaa watu, haya ndiyo mafunzo ya Chapa halisi ya kitabu cha Fadhaa-il A'maal na vitabu vyengine vya mambo ya uzushi- vinavyotumiwa na Jamaa'ah at-Tableegh.

2) 'Aqeedah ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuwa Haadhir wa Naadhir (kuwepo na kuhudhuria daima) inavyofunzwa katika Fadhaa-il A'maal

'Aqeedah nyengine mbovu iliyotambaa katika fahamu za Waislamu wengi na kufundishwa kwa bidii na Tableeghi Jamaat kwa kupitia Fadhaa-il A'maal ni kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni "Haadhir wa Naadhir" maana yake huwepo kila mahali na huwasaidia vipenzi vyake wakiwa kwenye dhiki.

Kulingana na Qur'aan Tukufu na Sunnah zilizo saheeh, hii ni 'Aqeedah mbovu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ambae kila Sifa njema ni yenye kumthubutukia Yeye amesema katika Takatifu (kama ilivyofasiriwa):

ذَٰلِكَ مِنْ أَنۢبَآءِ ٱلْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ ۖ وَمَا كُنتَ لَدَيْهِمْ إِذْ أَجْمَعُوٓا۟ أَمْرَهُمْ وَهُمْ يَمْكُرُونَ ﴿١٠٢﴾

"Hizi ni katika khabari za Ghayb (siri) Tulizokufunulia (Ewe Muhammad). Na hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao, hali (walipokuwa) wakifanya vitimbi vibaya". } [Soorah Yoosuf, Aayah 102]

Na pia, kama tungelikuwa na imani yakwamba mtume huwepo kila mahali basi kuna maana gani yake kufanya Hijrah na kwenda Madeenah kutoka Makkah, aondoke Madeenah na kuelekea Badr. Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) anapokuwepo Makkah huwa hayuko Taif na anapokuwepo Taif huwa hayuko Tabuk.

Wale wanaodai yakwamba Mtume ni Haadhir wa Naadhir wanatoa ushahidi wao kutokamana na kuonana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Moosaa (`alayhis-salaam) kwenye wingu wa sita wakati wa Mi'raaj na pia alipomuona anaswali katika kaburi lake. Jawabu letu kwa watu hawa tunasema: Hii ni miujiza ya Mwenyezi Mungu. Kutokamana na Hikma Zake zisokifani, Ameonyesha Alama Zake kwa Mtume Wake (sal-Allaahu `alayhe wa sallam). Akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) katika Qur'aan (kama ilivyofasiriwa):

ٱلَّذِى بَـٰرَكْنَا حَوْلَهُۥ لِنُرِيَهُۥ مِنْ ءَايَـٰتِنَآ ۚ

"...ambao (tumeubariki na) tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake (Tulimpeleka hivyo) ili tumuonyeshe (yeye Muhammad (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam)) baadhi ya Alama Zetu (Ishara, mafunzo, dalili, n.k). [Soorah Israa, Aayah 1]

Yeyote akatikae mkono kawaida hutoka damu, lakini Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) aliyafanya maji mara mbili kutiririka kutoka kwenye mikono ya Mtume wake. Lakini siku alipopata majaraha akiwa Uhud, Mtume (sal-Allaahu `alayhe wa sallam) alitiririkwa na damu, na sio maji wala muangaza.

Miujiza ni kwa makusudio maalum na ni kwa nyakati fulani. Haiwezi kutumiwa kama ushahidi, haswa katika mas-ala ya 'aqeedah. Kwahivyo 'aqeedah ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu yakwamba yeye ni Haadhir wa Naadhir (kuwepo kilamahali) ni urongo. Lakini kitabu hichi cha Fadhaa-il A'maal kinafundisha 'aqeedah hii si chini ya mahali kumi haswa kwenye Fadhaa-il Durood.

Hebu tusomeni wenyewe:
Akaeleza Muhammad Zakaria Kandalvi katika ukurasa wa 84, Tukio la (Hikayat)- 4 Fadhaa-il Durood: "Minhaj al-Hasanat akadondoa kutoka kwenye kitabu 'Fajr Munir' cha Ibn Fakhafi yakwamba walii mmoja "buzurg" (iliyo na maana sawa na Mzee) aliekuwa akiitwa Moosaa Darir alietoa kisa chake: Nilikuwa kwenye jahazi lililoanza kuzama, mara usingizi ukanichukua na hapo akanijia Mtume wa Mwenyezi Mungu nikiwa katika hali hiyo, akanifundisha mimi niwaamrishe watu kwenye jahazi hilo wasome durood (kumswalia Mtume) mara 1000. Tulipofikisha idadi ya mara 300 tu, jahazi likarudi katika hali yake ya Usalama".

Jahazi linapo-gharikika na kutaka kuzama, abiria husikia usingizi au hutaharuki? Kisa hiki kinaweza kusamehewa yakwamba kilikuwa ni ndoto, lakini riwaya ifuatayo itakuchukiza; soma yalio katika fikra za wanavyuoni wa Deobandh.

Fadhaa-il Durood, uk.109, Tukio la (Hikayat) - 46:

"Akatuhadithia Haafidh Abu Na'eem kutoka kwa Sufyaan ath-Thawree yakwamba: Siku moja mimi (Sufyaan) nilikuwa nikitembea mara nikamuona kijana mmoja aliekuwa akisoma durood kila anapochukua hatua. Nikamuuliza, "Jee amali hii unayoifanya wewe, ina msingi wowote (au ni kitendo chako tu wewe mwenyewe)?" Akaniuliza, "Wewe ni nani?" Nikamjibu, "Mimi ni Sufyaan." Kisha akaniuliza, "Sufyaan wa Iraq?" Nikamjibu, "Ndie." Kisha akaniuliza tena, "Ni ilimu ya aina gani ya Mwenyezi Mungu uliyonayo?" Nikamjibu, "Huutoa usiku kutoka katika mchana na mchana kutoka katika usiku na anau-umba uso wa mtoto mchanga akiwa katika uzao." Akanijibu, "Basi wewe hujui chochote." Kisha nikamuuliza, "Wewe unamjuaje Mwenyezi Mungu?, ni nini hii durood yako?" Akanijibu, "Niliwahi kwenda na mamangu kuhiji Makkah na mamangu akafa huko, uso wake ukawa mweusi na tumbo lake likafura mpaka nikafahamu yakwamba amewahi kufanya madhambi makubwa ya hatari. Nikainua mikono yangu kuomba du'aa Kwa Mwenyezi Mungu ndipo nilipo-ona kutoka katika muelekeo wa Hijaz kukatokeza kiwingu ambacho ndani yake akazuka mtu. Akaeka mikono yake kwenye uso wa mamangu mara uso ukang'ara na akampapasa tumbo kwa mikono yake na kufura kukapotea. Nikamuuliza yeye alikuwa ni nani alie-muuguza mamangu na mimi kutoka katika shida tulizokuwa nazo. Akanijibu, "Mimi ni Mtume wako Muhammad. Kisha nikamuomba anipe nasiha. Akaniamrisha nimpelekee durood (maamkuzi) katika kila hatua."

Ni urongo wa kutisha ulioje huu na matusi juu ya Mtume wetu tumpendae! Zakaria Kandalvi ataka sisi tuamini yakwamba mjumbe wa Mwenyezi Mungu yu-hai na yuazunguka kusaidia watu. Na ni utovu wa adabu ulioje huu aliouzua! Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam), ambae mkewe 'Aaisha aliemsifu kuwa alikuwa na hayaa' zaidi kuliko mwanamke bikra (ambae hajawahi kuingiliwa) aliejisitiri), amemkanda mwanamke sehemu yake ya uso na tumbo?! Astaghfirullah.

Ningelipendelea kuwauliza wanavyuoni wa Deobandh na Tableeghi Jamaat nzima: Hizi shughuli za uokozi za Mtume zimesimama au bado zaendelea mpaka sasa. Kwanini basi haji akawaokoa Waislamu wa Kashmir, Palestine na Chechnya? Nawauliza watu wa Tableeghi yakwamba Mtume alikuwa wapi wakati 'Umar alipouwawa, na 'Uthmaan alipouwawa na pia 'Alee alipouwawa?

Ole wao! Ndugu yangu Muislamu, unauona urongo na ukosefu wa adabu anaofanyiwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa jina la mapenzi, kwa jina la kuutumikia Uislamu. Kwa watu wenye kusema urongo kama hao, sisi tunawaambia yeyote mwenye kumzulia Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam)kwa kukusudia basi na achukue nafasi yake motoni. Na hayo ni makaazi maovu mno! Lakini bado hatujamaliza huo urongo. Akaendelea kusema Zakaria Kandalvi:

1) Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) anambusu soofi mwenda-wazimu (Fadhaa-il Durood, Tukio la - 42, uk.102)

2) Muhammad (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) kutoka angani akiwa juu ya wingu ateremka na kipande cha mkate mkononi kwa min-ajil ya kuwalisha "wafuasi wake wema" (Fadhaa-il Durood, Tukio la - 48, uk.110)

3) Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, alie mwisho wa Mitume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) ang'oa ndevu zake na kumpa mtu anaekata roho ili amtibu. (Fadhaa-il Durood, uk.110, Tukio la - 48)

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) Atulinde na uzushi kama huo, utovu wa adabu na upuzi dhidi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) na atujaalie ni miongoni mwa wanywaji kutoka katika Haud (ziwa la) al-Kawthar.

'Akatuhadithia 'Alee (Radhiallahu 'anhu) yakwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) amesema: **"Musinizulie mimi, kwani yeyote atakae-nizulia mimi naaingie motoni".** [Bukhaaree V.1/106].

Zubayr Abu Abdullaah akapokea yakwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) amesema: **"Yeyote mwenye kunizulia mimi kwa kukusudia basi na atafute makaazi yake motoni"**. [Bukhaaree V.1/107].

Salamah akapokea yakwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) amesema: **"Yeyote mwenye kusema kunihusu mimi kitu ambacho sikukisema basi na ajitafutie makaazi yake motoni"** . [Bukhaaree V.1/109].

3) Usambazaji wa 'Aqeedah yakwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) yu-hai katika kaburi lake, yuatusikia na ana ilimu ya yaliofichamana.

Muandishi wa Fadhaa-il A'maal, Muhammad Zakaria Kandalvi anaamini na anataka kueneza mafundisho yake yakwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu:

a) Yuko hai katika kaburi lake na anatusikiya sisi;

b) Ana ilimu ya yaliofichamana.

Kwa Muislamu wa Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah na alie juu ya 'aqeedah ya wema wetu waliotutangulia kuamini uvumi kama huu si chochote isipokuwa Kufr na Shirk. Yanapingana wazi-wazi na Qur'aan Takatifu na Sunnah zilizo saheeh za Abul-Qaasim (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam).

Kuhusiana na habari yakwamba yeye yuko hai na anatusikiliza sisi, Neno la Mwenyezi Mungu, maneno ya kuaminika zaidi yametubainishia ukweli. Akasema Mwenyezi Mungu katika Qur-aan Tukufu (kama ilivyofasiriwa):

وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّن قَبْلِكَ ٱلْخُلْدَ ۖ أَفَإِين مِّتَّ فَهُمُ ٱلْخَٰلِدُونَ ﴿٣٤﴾
كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ ٱلْمَوْتِ ۗ وَنَبْلُوكُم بِٱلشَّرِّ وَٱلْخَيْرِ فِتْنَةً ۖ وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٥﴾

"Nasi hatukumfanya mwanadamu yoyote wa kabla yako (Ewe Muhammad) aishi milele. Basi kama ukifa wewe wao wataishi milele? Kila nafsi itaonja mauti, na tunakufanyieni mitihani kwa (mambo ya) shari na ya kheri; na kwetu (nyote) mtarejeshwa" [Soorah al-Anbiya, Aayahs 34-35]. Na pia: **"Kwa yakini wewe (Ewe Muhammad) utakufa na wao pia (vilevile) watakufa"** [Soorah Az-Zumar, Aayah 30]

Na ni nani atakaesahau mawaidha ya kihistoria ya Abu Bakar as-Siddeeq (radhiallaahu 'anhu) isipokuwa wazushi! kwa kweli alisema: ((Na sasa, kwa yule anaemuabudu Muhammad (sallallaahu `alayhi wasallam), basi Muhammad ameshakufa. Lakini kwa yule anaemuabudu Mwenyezi Mungu, Yeye ni wa milele na wala hafi)) Akasema Mwenyezi Mungu (kama ilivyofasiriwa):

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ ٱلرُّسُلُ ۚ
أَفَإِيْن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ ٱنقَلَبْتُمْ عَلَىٰٓ أَعْقَـٰبِكُمْ ۚ وَمَن يَنقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ
فَلَن يَضُرَّ ٱللَّهَ شَيْـًٔا ۗ وَسَيَجْزِى ٱللَّهُ ٱلشَّـٰكِرِينَ ﴿١٤٤﴾

"Na hakuwa Muhammad ila ni Mtume tu. Wamepita kabla yake Mitume (wengi kabisa). Akifa au akiuawa ndio mtarudi nyuma (kwa visigino vyenu), muwe makafiri kama zamani? Na atakaerudi nyuma kwa visigino vyake hatamdhuru Mwenyezi Mungu chochote. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wanaomshukuru. [Soorah Aal-'Imraan, Aayah 144] Akasema Ibn al-Musayyib yakwamba 'Umar amesema: ((Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, pindi nilipomsikia Abu Bakar akiieleza habari hiyo, nilianguka chini. Nilijihisi kama kwamba miguu yangu haikuweza kunihimili mwili wangu kwahivyo nikazimia nilipomsikia akieleza habari hizo. Hapo ndipo nilipoamini yakwamba Muhammad (sallallaahu `alayhi wasallam) kweli amekufa)), [Bukhaaree, 2/640, 641]

Inatakikaniwa ifahamike na kila Muislamu yakuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) haishi tena katika maisha haya ya duniani. Jambo hilo linatupeleka kwenye nukta ya pili tunayokusudia kuizungumza: Jee, Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) ana ilimu ya kujitegemea ya yalio fichamana?
Neno la Mwenyezi Mungu linasema:

وَعِندَهُۥ مَفَاتِحُ ٱلْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَآ إِلَّا هُوَ ۚ

"Na ziko kwake (Mwenyezi Mungu tu) funguo za siri; hakuna azijuae ila Yeye tu" [Soorah al-An'am, Aayah 59] .

قُل لَّا يَعْلَمُ مَن فِى ٱلسَّمَـٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ٱلْغَيْبَ إِلَّا ٱللَّهُ ۚ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ
يُبْعَثُونَ ﴿٦٥﴾

Sema: "Hakuna aliyoko katika mbingu na ardhi ajuaye Ghayb (yasiyotokea) ila Mwenyezi Mungu; nao (hao wanaowaabudu) hawajui ni lini watafufuliwa, (watayajua mengineyo?)." [Soorah an-Naml, Aayah 65]

قُل لَّآ أَمْلِكُ لِنَفْسِى نَفْعًا وَلَا ضَرًّا إِلَّا مَا شَآءَ ٱللَّهُ ۚ وَلَوْ كُنتُ أَعْلَمُ ٱلْغَيْبَ
لَٱسْتَكْثَرْتُ مِنَ ٱلْخَيْرِ وَمَا مَسَّنِىَ ٱلسُّوٓءُ ۚ إِنْ أَنَا۠ إِلَّا نَذِيرٌ وَبَشِيرٌ
لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿١٨٨﴾

© Manhaj ya Salafi 2002. www.manhajyasalafi.com

Sema: "Sina mamlaka ya kujipa nafuu wala ya kujiondolea madhara ila apendavyo Mwenyezi Mungu; na lau kama ningalijua ghaibu ningejizidishia mema mengi; wala isingalinigusa dhara; mimi si chochote ila ni muonyaji na mtoaji wa habari njema kwa watu wanaoamini." [Soorah al-A'raaf, Aayah 188]

قُل لَّآ أَقُولُ لَكُمْ عِندِى خَزَآئِنُ ٱللَّهِ وَلَآ أَعْلَمُ ٱلْغَيْبَ وَلَآ أَقُولُ
لَكُمْ إِنِّى مَلَكٌ ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰٓ إِلَىَّ ۚ قُلْ هَلْ يَسْتَوِى ٱلْأَعْمَىٰ
وَٱلْبَصِيرُ ۚ أَفَلَا تَتَفَكَّرُونَ ﴿٥٠﴾

Sema: "Mimi sikwambieni kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu (nikakupeni mnayoyataka;) wala (sikukwambieni kuwa) najua mambo ya siri (ya Mwenyezi Mungu nikakubainishieni yatakayokufikieni katika biashara zenu na mengineyo kama mlivyotaka nikwambieni), wala sikwambieni kuwa Mimi ni Malaika (hata mkanambia: 'Kwa nini unakula na kuoa'). Mimi sifuati ila yale yaliofunuliwa kwangu." Sema: "Je, kipofu na mwenye macho huwa sawa? Basi je, hamfikiri?" [Soorah al-An'aam Aayah 50]

ذَٰلِكَ مِنْ أَنۢبَآءِ ٱلْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ ۚ وَمَا كُنتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يُلْقُونَ أَقْلَٰمَهُمْ
أَيُّهُمْ يَكْفُلُ مَرْيَمَ وَمَا كُنتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يَخْتَصِمُونَ ﴿٤٤﴾

"Hizi ni khabari za ghaibu tunazokufunulia; nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa kalamu zao ndani ya maji (kwa kura, wajue) nani wao atamlea Maryamu, na hukuwa nao walipokuwa wakishindana" [Soorah Aal 'Imraan Aayah 44]

وَلَآ أَقُولُ لَكُمْ عِندِى خَزَآئِنُ ٱللَّهِ وَلَآ أَعْلَمُ ٱلْغَيْبَ وَلَآ أَقُولُ إِنِّى مَلَكٌ
وَلَآ أَقُولُ لِلَّذِينَ تَزْدَرِىٓ أَعْيُنُكُمْ لَن يُؤْتِيَهُمُ ٱللَّهُ خَيْرًا ۖ ٱللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا
فِىٓ أَنفُسِهِمْ ۖ إِنِّىٓ إِذًا لَّمِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٣١﴾

"Wala sikuambieni kuwa nina khazina za Mwenyezi Mungu; wala kuwa mimi najua mambo ya ghaibu; wala sisemi, 'Mimi ni Malaika;' wala sisemi kwa wale ambao yanawadharau macho yenu kuwa Mwenyezi Mungu hatawapa kheri. Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo katika nafsi zao. (Nikisema hivi) hapo bila shaka nitakuwa miongoni mwa madhalimu." [Soorah Hood, Aayah 31]

"Hizi ni katika khabari za siri tunazokufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii (Qur'aan kuteremshwa). Basi subiri; hakika mwisho (mwema) utawathubutikia wanao-mcha Mungu." [Soorah Hood, Aayah 49]

ذَٰلِكَ مِنْ أَنۢبَآءِ ٱلْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ ۖ وَمَا كُنتَ لَدَيْهِمْ إِذْ أَجْمَعُوٓا۟ أَمْرَهُمْ
وَهُمْ يَمْكُرُونَ ﴿١٠٢﴾

"Hizi ni katika khabari za siri tunazokufunulia. Na hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao, hali wakifanya vitimbi vibaya." [Soorah Yoosuf, Aayah 102]

وَيَقُولُونَ لَوْلَآ أُنزِلَ عَلَيْهِ ءَايَةٌ مِّن رَّبِّهِۦ ۖ فَقُلْ إِنَّمَا ٱلْغَيْبُ لِلَّهِ
فَٱنتَظِرُوٓا۟ إِنِّى مَعَكُم مِّنَ ٱلْمُنتَظِرِينَ ﴿٢٠﴾

Na wanasema: "Kwa nini haikuteremshwa juu yake kutoka kwa Mola wake miujiza (tunayoitaka)?" Basi sema: "Ilimu ya mambo yasiyo-onekana iko kwa Mwenyezi Mungu. Basi ngojeni; na mimi ni pamoja nanyi katika wanaongoja." [Soorah Yoonus, Aayah 20]

قُل لَّا يَعْلَمُ مَن فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ٱلْغَيْبَ إِلَّا ٱللَّهُ ۚ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ
يُبْعَثُونَ ﴿٦٥﴾

Sema: Hakuna aliyoko katika mbingu na ardhi ajuaye Ghayb (yasiyotokea) ila Mwenyezi Mungu; nao (hao wanaowaabudu) hawajui ni lini watafufuliwa, (watayajua mengineyo?)." [Soorah an-Naml, Aayah 65]

Yeyote mwenye kuwa na Imani kinyume na hayo yaliokwisha elezwa hapo juu basi huyo amezama kwenye upotofu na kwa hakika kujiambatanisha na Imani hiyo humuingiza mtu kwenye Kufr na Shirk kwani inapinga moja ya nguzo za Tawheed!

Ndio, Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) katika nyakati fulani, alipewa 'Ilmu ya yaliyo kufichamana, lakini hayo hayakutoka kwake, yametoka kwa Mwenyezi Mungu Aliyempa yeye 'Ilmu hii alipokuwa katika hali au nyakati fulani kama miujiza na alama za kuthibitisha ukweli wake kama mjumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

عَٰلِمُ ٱلْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِۦٓ أَحَدًا ﴿٢٦﴾ إِلَّا مَنِ ٱرْتَضَىٰ مِن رَّسُولٍ فَإِنَّهُۥ
يَسْلُكُ مِنۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِۦ رَصَدًا ﴿٢٧﴾

"Yeye ndiye Mjuzi wa siri; wala hamdhihirishii yoyote siri yake. Isipokuwa Mtume wake aliyemridhia. Huyo yeye humwekea walinzi mbele yake na nyuma yake.
[Soorah Jinn, Aayah 26-27]

Lakini anaedai yakwamba Mitume na Manabii wana 'Ilmu ya yaliyo fichamana ya kujitegemea wao wenyewe, basi huyo yupo juu ya Ukafiri, na ajilinde na Mwenyezi Mungu. Lakini wazushi, kama viongozi wa Jamaa'at-ut-Tableegh wanaoruhusu upotofu huu uendelee kufundishwa na ubakie, hawafahamu, au hujidai kama kwamba hawajui mambo yaendeleayo, ambayo yalio wazi kama muangaza wa mchana kwenye Kitabu Kitakatifu cha Mwenyezi Mungu.

Isitoshe hiyo, muandishi huyu wa Fadhaa-il A'maal Zakaria Kandalvi amezua uwongo mkubwa zaidi, na kumkosea adabu Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam), jambo ambalo pengine hata makafiri hawajawahi kufanya. Ameandika Kandalvi katika ukurasa wa 115, Tukio la (Hikayat) - 50, Fadhaa-il Durood (Tukio la mwisho la Hikayat katika Fadhaa-il A'maal, Vol.I). Anahadithia kisa cha mtu asiejulikana aitwae "Maulana Jami".

"Siku moja Maulana Jami alifunga safari kuelekea Hajj na akanuilia kusimama kwenye kaburi la Mtume wa Mwenyezi Mungu ili asome mashairi kwenye kaburi. Alipokamilisha Hajj, akasafiri kuelekea Madeenah. Ameer wa Madeenah akamuona Mtume kwenye ndoto na Mtume akamuamrisha yakwamba asimruhusu Jami kuingia Madeenah. Yule Ameer akaeka ulinzi mkali lakini ujabari na "Ishq" (fahamu: Neno ishq hutumiwa kwa yale mapenzi yenye kuandamana na tamaa mbaya ya uzinifu!) kwa ajili ya kumzuru Mtume ukamfanya asijali chochote na akaendelea na safari yake hadi Madeenah. Ameer nae akamuota tena Mtume na Mtume akamuamrisha yakwamba asimruhusu Jami kuingia Madeenah. Ameer akawabumburusha watu wake mpaka wamkamata jami. Baada ya kukamatwa akavurumizwa jela. Kisha kwa mara ya tatu Ameer akamuota tena Mtume nae Mtume akampasha habari yakwamba (Jami) si muhalifu lakini alikuwa ametunga mistari michache ya mashairi na amekusudia kuja kunisomea katika kaburi langu na lau kama angelifanya hivyo (yaani: kuweza kuyasoma hayo mashairi kwenye kaburi langu) basi mkono wangu ungelitokeza nje ya kaburi kumsalimia na jambo hilo lingelizua fitnah. Kwahivyo, Jami akapewa heshima kubwa, akatolewa jela na kuachwa huru."

Akaendelea Muhammad Zakaria: "Sina shaka yoyote katika kukisikiliza kisa hiki lakini nashindwa na fahamu zangu dhaifu na magonjwa niliyo nayo katika kukumbuka niliipokea kutoka katika kitabu gani. Ikiwa yoyote katika wasomaji atakiona kisa hicho katika kitabu chochote katika uhai wangu basi tafadhali na anijulishe na ikiwa ni baada ya kufa kwangu, basi tafadhali ongeza kumbukumbu chini ya kisa hicho kama maandishi ya chini "footnote"."

Astaghfi-rullaah! Ni aibu ilioje hii, uwongo wa kukusudia! Huyu Zakaria hana khofu anapozua urongo wa aina hii na haswa kumzulia Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) kwa njia ya kutuhuzunisha kama tunavyo-ona hapo juu? Asema hawezi kukumbuka amekitoa wapi kisa hicho?! Na kisha akawahimiza wafuasi wake wampashe habari iwapo ameghafilika! Basi ni kwa nini kukisimulia hapo mwanzo - Huku ni kuzua urongo wa dhahiri ulio wazi kwa Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) - licha ya mambo ya upotofu yaliomo ndani yake!!

Abu Hurayrah (Radhiallahu 'anhu) amepokea kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) kuwa amesema: **"Inatosha kumfanya mtu kuwa mrongo anapohadithia kila anachosikia"** [Imepokewa na Imaam Muslim] Na pia akatuhadithia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam): **Siku ya mwisho itakapowadia, watakuja ma-Dajjaal, waongo, watakao-wasimulia ahaadeeth ambazo**

hamujawahi kuzisikia nyinyi wala mababu zenu. Basi tahadharini na mujitahadhari sana, wasije wakawapoteza na kuwatia kwenye fitnah" [Saheeh Muslim na Musnad Ahmad, nayo ni Saheeh]

Na Ibn Hibbaan akaziweka ahadeeth zinazo kataza kumzulia Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) chini ya mlango wenye kichwa kisemacho "Kwa mwenye kukinasibisha kitu chochote kwa al-Mustafaa na akawa hajui yakwamba ni saheeh, basi atastahiki kuingia motoni", na kisha akaitaja hadeeth ya Abu Hurayrah: **"Yoyote atakaenizulia mimi uwongo, basi na ajitafutie makaazi yake motoni"** [Saheeh Ibn Hibbaan, uk.27]

Basi hii ndio hali na msimamo wa "Muhaddith", alie "Kielelezo cha Ulimwengu" (!!!), Zakaria Kandalvi?! Katika kuongezea, ambao ni uovu wa mwisho, jamani hii si Shirk kudai yakwamba Mtume (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) ana ilimu ya kujua nia za watu kutoka kaburini mwake. Ni nani ajuae nia za watu? Allaah! Ni aqeedah gani hiyo mbovu ifundishwayo hapo!

Lakini Zakaria Kandalvi hakukoma hapo. Ilimbidi adhihirishe Utukufu na utawa wake wa ki-Soofi. Endelea kusoma kwenye Tukio hilo-hilo: "Syed Ahmad Refai ni "buzurg" mashuhuri sana (Mzee, lakini na ifahamike kuwa ni shekhe) na alikuwa ni miongoni mwa ma-Soofi wakubwa. Kisa chake kinajulikana sana pindi alipokwenda Hajj katika mwaka wa 555H na akasimama karibu na kaburi la Mtume (akiwa Madeenah) na akasoma mistari miwili ya mashairi, basi mkono wa Mtume ukajitokeza nae akaubusu." Mimi nashuku yakuwa mambo haya yameandikwa na Muislamu mwenye akili timamu. Urongo kama huo, uzushi na ukosefu wa adabu yamkinika kutoka kwa adui wa mafundisho yalio saheeh ya kisawa-sawa ya Uislamu, lakini hayo yametoka kwa "Shaykh al-Hadeeth", "Mjuzi wa Mwenyezi Mungu", "Kielelezo cha Ulimwengu" Muhammad Zakaria Kandalvi!

Ndugu zangu na Dada zangu Waislamu: Mushavisoma hivyo visa vya Shirk, uzushi na urongo juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Hayo ni baadhi chache tu miongoni mwa visa chungu nzima vya urongo vilivyofika kilele katika mijalada miwili ya Fadhaa-il A'maal. Hayo tuliyo-yapitia ni Fadhaa-il Durood peke yake. Kuna Fadhaa-il Hajj, Sadaqa, Dhikr, Salaah na Ramadhaan tumeya-acha. Inshaa-Allaah, hiyo Shirk iliyoko kwenye milango hii itafichuliwa kulingana na Qur'aan na Sunnah zilizo-Saheeh.

Basi jitahadharini ndugu zangu na Dada zangu! Jitahadharini na kukaa pamoja na Jamaa'at-ut-Tableegh, au kutoka nao na kuwasikiliza usije na wewe ukazama kwenye shimo la Shirk na Bid'ah, kwani mambo hayo ni yenye kufisidi nyoyo na fahamu na kukuelekeza kwenye upumbavu na ujinga. Badala yake fuata nasiha za watangulizi wetu wema: Al-Fudayl bin 'Iyaad (f. 187H) amesema: ((Nilipambana na watu walio bora, wote hao walikuwa ni watu wa Sunnah na walikuwa wakikataza kuwa pamoja na wazushi)), [Imepokelewa na al-Laalikaa'ee (no.267)] . Nae al-Hasan al-Basree (f. 110H) amesema: ((Usikae na wazushi na watu wa Hawaa, usijadiliane nao na wala usiwasikilize)), [Imepokewa na ad-Daarimee katika Sunan yake (1/121)]

Imepokewa kutoka kwa Aboo Qulaabah, aliesema: ((Usikae nao na wala usijumuike nao kwani nina shaka huwenda wakakuzamisha kwenye upotofu wao na kukuzengua akili kuhusiana na mengi ulokuwa ukiyajua)), [Laalikaa'ee no. 244] Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) Atuthibitishe juu ya Tawheed na Sunnah za Mtume wake (Sal-Allaahu `alayhi wa sallam) na Atuepushe mbali kabisa na hizaya za Shirk na Bid'ah na mafundisho ya Tableeghi Jamaat. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) Aija'alie shughuli hii ya ukusanyaji wa makala haya yawe ni kwa ajili ya kutafuta Radhi zake na Anisamehe makosa yangu. Sisi sote ni Wake Yeye na Kwake yeye tutarudi.

Mtumwa wa Mwenyezi Mungu, Abu Muawiya as-Sabt
15 Dhul-Hijjah,
1421 H Jumamosi 19 March, 2001
Imetengenezwa na kufanyiwa marekebisho na Abu Iyaad.